# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL8

# KISWAHILI PAPER 1 ANSWER

1. (i) Hii ni barua rasmi. -Ina anwani mbili na tarehe.

(ii)Kuna mtajo:kwa Bw/Bi

(iii)Kusudi:**MINT/KUMB/KUH:MAOMBI YAKAZ**I.

(iv)Uraia wako.

(v) Jinsia/uana wako.

(vi)Umri wako.

(vii) Masomo.

(a) Shule ya msingi(wapi?ukapata alama ngapi?)

(b) Shule ya sekondari (wapi?ukapata nini?)

(viii)Wadhifa katika shule ya msingi.

(ix)Wadhifa katika shule ya sekondari

(x) Mafunzo ya kazi (wapi?lini?ukapata cheti kipi?)

(xi) Wadhifa katika chuo cha mafunzo.

(xii)Kazi –ulifanya wapi?lini.

(xiii) Ujuzi-miaka mingapi?

(xiv) Uraibu-unapenda nini?

(xv) Tamati.

- Ndimi wako mwaminifu,

- Sahihi.
- Jina mahsusi
- Cheo chako.(si lazima)

xvi) Warejelewa. - Wawe wawili na anwani au simu zao. * Mtahiniwa akipotoka kimtindo :apoteze alama 4.

2. Hii ni insha ya mjadala.

**Faida ya serikali ya ugatuzi.**

(i) Ajira nyingi zimezalishwa.

(ii) Rasimali kutumiwa na wananchi wenyewe.

(iii)Miundo msingi kuboreshwa.

iv) Maendeleo kusawazishwa kote nchini.

(v) Utawala kuwa karibu na wananchi.

(vi) Kuleta huduma muhimu karibu na watu.

(vii) Kushirikisha jinsia zote uongozini.

(viii) Usalama umeimarishwa.

Hasara za serikali ya ugatuzi

(i) Kuongezeka kwa kodi.

(ii) Gharama ya maisha imepanda-watawala ni wengi.

(iii)Tofauti za kimaendeleo.

(iv) Zimekuza hisia za kikabila.

(v) Mkanganyo kati ya serikali kuu na majimbo.

(vi) Majimbo yasiyo na rasimali ya kutosha yamebaki nyuma

(vii) Mapendeleo katika kutoa ajira.

(viii) Kujiuzulu kwa watalaamu, n.k

**TANBIHI**

*Hoja za kila upande zisipungue tano. *Mtahini ahakikishe hoja zingine za mtahiniwa.

**3. Udongo Uwahi ungali maji.**

i) Hii ni insha ya methali.

(ii) Mtahiniwa atunge kisa kinachooana na methali

(iii)Mtahini akamilishe kisa kwa kutoa funzo.

Anaweza kumaliza na methali iyo hiyo.

4. **Insha ya mdokezo.**

(i) Mtahiniwa amalize insha kwa maneno aliyopewa.

(ii) Aonyeshe sababu ya kutamani kuona babake.

(iii)Ajihusishe moja kwa moja.

(iv) Aonyeshe sababu iliyopelekea asimwone babake tena. *Mtahiniwa akipotoka apate alama 2/20

**NAMANA YA KUTUZA**

1. **Maki 01- 05**
    - Insha haileweki kwa vyovyote.

- Lugha ni hafifu sana.
- Lugha isiyo sahihi-ukosefu wa ubunifu,makosa ya kisarufi na hijai,mtindo mbaya,n.k

2. **Maki 06 -10**

- Mawazo yamewasilishwa lakini kwa njia isiyoeleweka kikamilifu.
- Mada haijaendelezwa kikamilifu.
- Amepotoka hapa na pale.
- Kujirudiarudia.
- Makosa ya kisarufi/hijai.

3. **Maki 11-15**

- Mtahiniwa amedhihirisha kuimudu lugha.
- Ametumia miundo sahihi ya sentensi.
- Ubunifu umedhihirika.
- Insha inaeleweka na ina mtiririko.

4. **Maki 16 -20**

- Insha ina mtiririko.
- Maudhui sahihi yamekuzwa.
- Kuna ubunifu.
- Ametumia tamathali za usemi.
- Mawazo yamewasilishwa kwa mpangilio unaovutia.
- Makosa yote yasizidi matano.

**MAMBO YA KUANGALIA**.

(i) Urefu.

(ii) Hati.

(iii)Uakifishaji.

(iv) Mtindo ya kuandika baadhi ya herufi ambayo si sahihi.

(v) Unadhifu wa kazi.

(vi) Sura ya insha.

**MAKOSA YA HIJAI** (h)

(i) Kutenganisha neno k.m aliye kuwa.

(ii) Kuunganisha maneno k.m kwasababu.

(iii)Mwendelezo mbaya wa neno.

iv) Kuandika maneno kifupi.

(v) Kukatia neno kwenye konsonanti//kulikata mwishoni bila kuweka kistari n.k.

**MAKOSA YA SARUFI** (s)

(i) Kuakifisha vibaya.

(ii) Kutumia herufi kubwa ama ndogo mahali si pake.

iii)Matumizi mabaya ya ngeli,nyakati na mnyambuliko.

(iv) Kuacha au kuongeza neno katika sentensi k.m kwa kwa n.k.